

PARLIAMENT OF KENYA

JOINT SITTING OF THE NATIONAL ASSEMBLY AND THE SENATE

THE HANSARD

*(Special Sitting of Parliament convened via
Kenya Gazette Notices Nos.4199 and 4200 of 3rd May, 2021*

Wednesday, 5th May, 2021

*Parliament met at Fifty minutes past two O'clock
in the National Assembly Chamber, Main Parliament Buildings*

ARRIVAL OF HER EXCELLENCY THE PRESIDENT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

[Her Excellency the President of the United Republic of Tanzania (Hon. Samia Suluhu Hassan escorted by the Speaker of the Senate (Hon. Lusaka) and the Speaker of the National Assembly (Hon. Muturi) entered the Chamber at Fifty minutes past two O'clock accompanied by the Maces of both Houses]

(The two Maces were placed on the Table)

PRAYER

CONVOCATION

MKUSANYIKO WA KIKAO MAALUM CHA BUNGE

Spika wa Seneti (Mhe. Lusaka): Mheshimiwa Mtukufu Rais, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Bunge la Taifa, Mheshimiwa Justin Muturi na Waheshimiwa Wabunge.

Kuambatana na Kanuni ya Kudumu 25(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa na Kanuni ya Kudumu 26 (2) ya Kanuni za Kudumu za Seneti zinazohusu hotuba za Wageni Mashuhuri, Maspika wa Bunge walipokea ombi la kumruhusu Mheshimiwa Mtukufu Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye yuko hapa katika ziara rasmi ya kitaifa nchini Kenya, kuhutubia Kikao cha pamoja cha Bunge.

Disclaimer: *The electronic version of the Senate Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor, Senate.*

(Heko)

Waheshimiwa Wabunge, Maspika wa Bunge, wakiitikia ombi hilo, wameitisha Kikao hiki cha Pamoja cha Bunge. Nilitoa Arifa ya Kikao hiki cha pamoja kupitia Gazeti Rasmi la Serikali, Arifa Nambari 4200 ya tarehe 3 Mei, 2021 kwa Waheshimiwa Maseneta.

Hivyo basi, Waheshimiwa Wabunge, Kikao hiki maalum kimeitishwa kwa njia inayofaa.

Asanteni!

(Heko)

The Speaker of the National Assembly (Hon. Muturi): Your Excellency, hon. Samia Suluhu Hassan, President of the United Republic of Tanzania, hon. Speaker of the Senate, hon. Kenneth Lusaka; hon. Members of Parliament, distinguished guests, ladies and gentlemen; pursuant to provisions of Standing Order No.25(1) of the National Assembly Standing Orders relating to address by visiting dignitaries, I received a request to accord an opportunity to Her Excellency Samia Suluhu Hassan, President of The United Republic of Tanzania, who is on a State visit to Kenya on invitation by H.E. Hon. Uhuru Kenyatta, President of the Republic of Kenya and Commander in Chief of the Kenya Defence Forces, to address our Parliament.

Hon. Members, having acceded to the request, the Speaker of the Senate and I convened this Joint Sitting of the Houses of Parliament. Subsequently, I gave notice of the Joint Sitting through Kenya Gazette Notice No.4199 dated 3rd May, 2021 to the Members of the National Assembly. In this respect, Hon. Members, I declare this Joint Sitting of the Houses of Parliament properly convened.

(Applause)

Hon. Members, may I recognize the delegation of Cabinet Ministers and senior officials from the United Republic of Tanzania, who are accompanying Her Excellency the President and are also present in Parliament this afternoon.

May I also recognize Cabinet Secretaries and other senior officials from our Government, who are accompanying Her Excellency to Parliament today. These distinguished guests are seated in the Speaker's Room and others in the Diplomatic Boxes and the Speaker's Gallery.

Please, Hon. Members, join me in welcoming them to Parliament in our usual way.

(Applause)

Hon. Members and distinguished guests, as you are aware, since Independence up to until this afternoon, only one other visiting Head of State has had the honour of addressing a Joint Sitting of the Houses of Parliament of the Republic of Kenya. This was H.E. (Dr.) Jakaya Mrisho Kikwete, the then President of the United Republic of Tanzania, who addressed Parliament on Tuesday 6th October, 2015.

Disclaimer: *The electronic version of the Senate Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor, Senate.*

Today's Address by Her Excellency Samia Suluhu Hassan, President of the United Republic of Tanzania, will be the second address by a visiting Head of State.

(Applause)

Hon. Members, this is a clear attestation of the deep and special relations that our two countries enjoy and the high esteem with which our Parliament holds the Leadership and the people of the United Republic of Tanzania

Hon. Members, it is now my honour and privilege, to invite Her Excellency Samia Suluhu Hassan, President of the United Republic of Tanzania to address this Joint Sitting of Parliament of Kenya.

Welcome, Your Excellency!

(Applause)

ADDRESS BY VISITING DIGNITARY

ADDRESS BY H.E. SAMIA SULUHU HASSAN,
PRESIDENT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Samia Suluhu Hassan):
Mhe. Justin Muturi, Spika wa Bunge la Taifa; Mhe. Kenneth Lusaka, Spika wa Bunge la Seneti; Waheshimiwa wa Bunge la Taifa na Bunge la Seneti; viongozi mbalimbali wa Serikali wa Tanzania na Kenya mlio pamoja nasi; wageni waalikwa; mabibi na mabwana, habari za mchana!

(Heko)

Waheshimiwa Maspika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na uhai na kutupatia kibali kilichotuwezesha kukutana hapa siku ya leo. Niko na furaha kubwa leo kupata nafasi ya kuhutubia Kikao cha Pamoja cha Bunge la Taifa na Bunge la Seneti la Jamhuri ya Kenya.

Kabla sijaendelea, niruhusu nitangulize shukrani zangu kwako, Mhe. Kenneth Lusaka, Spika wa Bunge la Seneti, na, Mhe. Justin Muturi, Spika wa Bunge la Taifa, kwa kuitisha Kikao hiki cha Pamoja cha Bunge na kunialika mimi kuhutubia. Kupitia kwenu, ninawashukuru Waheshimiwa wabunge la Taifa na Bunge la Seneti, kwa kuridhia kwa kauli moja kufanyika kwa Kikao hiki. Asanteni sana!

(Heko)

Ninajiona mwenye bahati kubwa kupewa heshima hii adhimu na ya kipekee. Kama alivyosema Mhe. Spika, aliyewahi kuhutubia hapa ni Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, kutoka Tanzania na mimi ni wa pili. Ni bahati kubwa sana.

Disclaimer: *The electronic version of the Senate Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor, Senate.*

Ninatambua kwamba huu sio utaratibu wa kawaida wa Kenya. Sio kila Rais anayefanya ziara rasmi hupewa heshima hii ya kuhutubia Bunge, tena Kikao cha Pamoja cha mabunge yenu mawili. Wenzetu mna Bunge lenye *Chambers* mbili, sisi wenzenu tuko na Bunge moja tu.

Kwangu, itakuwa ndio mara ya kwanza kuhutubia *Chambers* mbili za Bunge kwa pamoja. Sio jambo ndogo na ni heshima kubwa iliyoje. Mmenipa heshima kubwa sana. Nimefarijika kuwa nimepata nafasi hii mwanzoni mwa uongozi wangu. Niseme kuwa kumbukumbu hii haitafutika kwenye maisha yangu. Asanteni sana!

(Heko)

Uamuzi wenu wa kunipa fursa hii ni kielelezo cha thamani na uzito ambao mnaupa uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi zetu mbili. Niwahakikishieni kuwa nasi tumeguzwa sana na heshima, upendo na ukarimu mkubwa ambao mmetuonyesha. Wema huacha deni na deni lake ni kulipwa kwa wema. Sisi Tanzania, tutalipa wema huu.

Waheshimiwa Maspika, Maseneta na Wabunge, sitatenda haki nisipomshukuru kipekee ndugu yangu, Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mhe. Uhuru Kenyatta. Rais Kenyatta ni miongoni mwa viongozi wa mwanzo kabisa walionipigia simu kunifariji mara tu baada ya kusikia taarifa ya kifo cha aliyekuwa Rais wetu mpendwa, Hayati Mhe. (Dr.) Magufuli.

Kama haikutosha, hakusita kukatiza ratiba yake na kufika yeye binafsi kushiriki nasi katika msiba wa kitaifa kule Dodoma. Siku ile, alitufariji sana kwa maneno yake na salamu zake za buriani kutoka kwa wananchi wa Kenya. Hatutasahau pia kitendo chake cha kutukumbusha umuhimu wa kuheshimu dini na imani za wengine.

(Heko)

Mhe. Uhuru Kenyatta alisitisha kuhutubia akiwa jukwaani, ili kupisha *adhan* iliyokuwa ikisomwa Msikitini imalizike na ndio akaendelea. Alituwachia gumzo na funzo kubwa sana kwetu. Alitumia jukwaa lile kunipongeza kwa kushika dhamana hii ya Urais ya Awamu ya Sita ya Tanzania. Aliahidi kunialika nchini Kenya mara baada ya kipindi cha maombolezo kumalizika.

Rais Kenyatta ni mtu wa kutimiza ahadi. Mara tu baada ya kumalizika kipindi cha maombolezo, alinitumia ujumbe maalum kuniona, ambao pia uliambatana na mwaliko wa kutembelea Kenya. Na mimi nimekuja Kenya kuitika wito wake.

Mimi na ujumbe wangu tumepata mapokezi mazuri sana toka tulipowasili Jijini Nairobi. Tumejisikia tuko nyumbani haswa. Tumepokewa kwa ukarimu mkubwa na hio ndio hulka, desturi na asili ya watu wa Kenya.

Nimebaini kuwa sehemu kubwa ya ujumbe nilioambatana nao, wanajua vichochoro vya Jiji la Nairobi. Wanajua nyama choma inapatikana wapi. Lakini kutokana na Korona, hawakuweza kujibamba. Nina wasiwasi nisije nikawabakisha nyuma.

(Kicheko)

Tunawashukuru kwa yote; mapokezi na ukarimu mkubwa.

Jana nilifanya kikao na Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta na ujumbe wake wa viongozi wa Serikali. Tumekuwa na mazungumzo mazuri yenye kuamsha matumaini makubwa kwa mashirikiano kati ya nchi zetu mbili kwa siku zijazo mbele yetu.

Hapakuwa na ugumu wala ukakasi wowote katika kufikia mwafaka wa mambo tuliyo kuwa tukijadiliana. Tumezungumza kwa kindugu sana. Kilichojitokeza wazi katika mazungumzo yale ni namna ambavyo nchi zetu mbili zinakubaliana katika mambo mengi kuliko yale machache sana tunayotofautiana.

Hata hayo machache tunayotofautiana, yenyewe hayakuwa na misingi imara ya tofauti ila ni mitazamo tu ya watu. Mitazamo nyingi ambayo inaleta ukakasi huchangiwa kutokana na kukatika kwa mawasiliano baina ya nchi zetu mbili. Sasa ili kuondoa mikakati hasi kati yetu, tumekubaliana kujenga na kuendeleza utamaduni wa kukutana mara kwa mara katika ngazi zetu mbali mbali. Ndugu na jirani wanaotembeleana hujenga ukaribu kuliko wale wasiotembeleana. Umbali hujenga mashaka na ukaribu huondosha mashaka hayo.

Waheshimiwa Maspika, Maseneta na Wabunge, kama nilivyosema, hii ni ziara yangu ya kwanza rasmi nchini Kenya tangu kushika wadhifa wa uraisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 19.03.2021.

Ipendeze kusema kuwa itaingia katika kumbukumbu za kihistoria kuwa Kenya ndio nchi ya kwanza kwa raisi wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya ziara rasmi. Nilikwenda Uganda kwa mathumuni maalumu ya kusaini mktaba.

(Heko)

Haikuwa ziara rasmi. Ziara yangu rasmi ya kwanza nimeanza na Kenya. Kwa lugha nyingine, mguu wangu wa kwanza kutoka nje kwa ziara rasmi umeanza Kenya.

Jana nilikaribiswa *Iftar* na Mheshimiwa Rais na baadaye tukawa na chakula cha usiku. Dua nyingi zilisomwa na baada ya kumaliza kusoma dua, mvua ilinyesha. Ilikuwa baraka sana. Mungu ameweka baraka kwenye ziara yangu na yale yote ambayo tumezungumza. Kwa hivyo, tumshukuru Mungu.

Uamuzi wangu wa kuja Kenya, kuwa nchi ya kwanza, sio wa bahati mbaya wala ni wa makusudi. Busara inaelekeza kuwa ukiwa mpangaji mpya kwenye eneo, lazima ujitambulishe kwa majirani.

(Kicheko)

Nami kwa sababu ni mpangaji mpya kwenye hizo nafasi, nimeonelea nije kwa majirani kujitambulisha na nimeanza na jirani wa Kenya ambaye ni jirani ndugu. Nilipata mialiko mingi lakini nilisema eti nianze na hapa. Sijaanza na Kenya kwa sababu ni karibu kijografia, bali ni kwa sababu ya umuhumi na nafasi ya Kenya kwa Tanzania.

Uhusiano wa Tanzania na Kenya ni wa kipekee sana. Ni uhusiano uliofungwa katika mafundo matatu. Fundo la kwanza ni undugu wa damu kati ya wananchi wetu wa pande mbili ambao hauwezi kutenganishwa na mipaka ya kuchorwa kwenye ramani.

Makabila ya pande mbili za mpaka yanaingiliana na watu wake ni wale wale wamoja. Tanzania inapakana na nchi nane, lakini ni nchi ya Kenya pekee ndio ambayo tunajamii nyingi zilizopo katika pande mbili za nchi zetu.

Kwenye Ukumbi huu wa Bunge, nadhani ndani hapa kuna akina Otieno, Boke, Namelok kama ilivyo Tanzania. Lakini pia kuna akina Kilonzo na Kioko kama ilivyo Tanzania.

(Kicheko)

Lakini zaidi, kuna Mohamed Faki Mwinyihaji ambaye ni Seneta wa Mombasa na jina lake ni jina safi la Kizanzibari. Kwa hivyo, hatuwezi kutengana. Hiyo ni mifano chache tu.

Fundo la pili ni historia. Kabla ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 1967, nchi zetu mbili hizi tayari zilisha kuwa chini ya *East Africa Common Service Organization (EACSO)* zikiwa chini ya utawala wa Kikoloni wa waingereza. Huduma zetu muhimu, miundo mbinu yetu na uchumi zetu, zilifuma pamoja kabla hata nchi zetu hazijapata uhuru.

Fundo la tatu ni jiografia. Mwenyezi Mungu amejalia nchi zetu mbili hizi kuwa majirani. Tuna mipaka ya baharini na mipaka ya ardhini. Na hata ekolojia yetu ni moja. Ndio kusema kuwa hata wanyama pori wetu ni ndugu na ni majirani. Kuna wale wanyama pori ambao huja kupata mimba Kenya na wanarudi kuzaa Tanzania.

(Kicheko)

Ingekuwa wanyama wana uraia, wangekuwa raia wa wapi? Wakitoka Serengeti, hao huingia Maasai Mara. Hata tausi wetu walioko Ikulu Tanzania, wana ndugu zao Ikulu ya Nairobi. Kwa hivyo, kama tausi na wanyama wana undugu, sisi wanadamu tunatengana wapi? Hatuna pa kutengana.

Kutokana na ukweli huo, ushirikiano wetu sio wa hiari bali ni wa lazima kutokana na kanuni ya uasili wa undugu ambao Mwenyezi Mungu ameumba. Ushirika na ujirani yote yanatufanya tuwe pamoja. Hali ya maumbile, hatuna uwezo wa kubadilisha. Iliyobaki ni tupendane au tuchukiane, tuzungumze au tununiane, hatuwezi kukwepa kutokana na mafundo hayo matatu tuliyowekwa nayo pamoja.

Tunategemeana kwa kila hali. Iwe heri au iwe shari. Iwe neema au dhiki, tunategemeana. Panapotokea ukame Tanzania, njaa inabisha hodi Kenya. Uzalishaji wa viwanda ukisimama Kenya, bidhaa zinakosekana Tanzania. Kwa hivyo, tunategemeana. Hivyo, hapana budi ila tupatane na tuelewane ili tuishi kwa pamoja kwa neema na furaha.

Waheshimiwa Maspika, Maseneta na Wabunge, binafsi huwa nashangazwa sana na wale ambao wanadhani eti Kenya na Tanzania ni washindani, kwa hivyo, uhusiano wetu unapaswa kuwa wakuhasimiana na kukamiana.

Disclaimer: *The electronic version of the Senate Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor, Senate.*

Nawashangaa wanaodhani kuwa Kenya pekee yake ama Tanzania pekee yake inaweza endelea bila mwenzake. Mbaya zaidi ni kule kuamini kwao ya kwamba hiyo inawezekana tu mmoja wetu kumuangusha mwenzake. Hawa ni watu wenye mioyo ya choyo, maono mafupi na akili mbovu.

Ni bahati mbaya kuwa watu hawa wapo katika pande zote mbili; Kenya na Tanzania. Hutokea pia wachache wao sana wakawa ni watumishi wa Serikali zetu na hata wanasiasa wa pande mbili za nchi zetu.

Bahati kubwa ni kuwa, sio wengi na ndiyo maana uhusiano wa nchi zetu mbili unatimiza miaka 56 sasa. Ukiwacha ule uwasili, lakini ule wa kiserikali ni miaka 56 sasa.

Kwangu mimi na katika awamu yangu ya uwongozi, nitahakikisha kuwa Kenya inabaki kuwa ndugu, jirani, mshirika wa mkakati na mbia. Kenya ni nchi ya tano kwa nchi zinazoongoza kwa uwekezaji nchini Tanzania na ndiyo nchi ya kwanza ndani ya Afrika inayoongoza kwa uwekezaji nchini Tanzania.

Nyuma ya mataifa makubwa kama Uingereza, Marekani, China na India, inakuja Kenya. Ya kwanza kituo chetu cha uwekezaji zinaonyesha ya kuwa hadi kufikia Machi, 2021, kuna miradi mingi tu ya Kenya inayotekelezwa Tanzania kama Tshs500,013,000 kutoka Kenya ambayo inatekelezwa Tanzania na kutoa ajira kwa Watanzania Tshs51,187,000 na kuchangia mapato ya kiasi cha US\$1.7 billion.

Sekta zinazoongoza kwa uwekezaji kutoka Kenya yaani uzalishaji viwandani, usafirishaji, kilimo, huduma, benki, ujenzi, rasilmali watu, madini, utalii na mali asili. Kutokana na uhusiano wetu mzuri, kampuni za Tanzania zimewekeza nchini Kenya lakini tumekuwa kwa uchache sana. Tuko kama kampuni 25 mpaka 30 zilizosajiliwa na mamlaka ya uwekezaji ya Kenya.

Miradi hiyo ina dhamani ya Kshs19.33 billion na kutoa ajira kwa raia kama 2,642. Kwa hivyo, Tanzania tuna deni kubwa kuja Kenya lakini pamoja na mapungufu hayo tuliyo nayo, bado tunawaalika Wakenya wengi zaidi waje Tanzania kuwekeza.

(Heko)

Tunawaalika kwa sababu Tanzania ina mambo mengi; ina rasilmali za kutosha, madini ya kutosha, ardhi kubwa na mambo mengi mengine, tunakosa mtaji. Kenya mna mtaji wa kutosha. Karibuni Tanzania.

Dhamira yangu ya kuja nchini Kenya ni kuzungumza na nyinyi na kuona namna gani Watanzania wataweza kufanya vizuri zaidi nchini Kenya. Mbali na uwekezaji, ushirikiano wetu kwenye sekta ya biashara nao ni mkubwa na umeendelea kushamiri siku hadi siku.

Usafirishaji wa bidhaa za Tanzania kwenda Kenya umeongezeka kutoka Tshs309.6 billioni mwaka 2017 hadi Tshs526.3 billioni mwaka 2020.

Kwa upande wa Kenya nayo iliongeza kiwango cha kuuza bidhaa zake nchini Tanzania kutoka Tshs420 billioni mwaka 2007 hadi Tshs571 billion mwaka 2020.

Hii inatusuta sisi viongozi na wanasiasa. Inatuonyesha kuwa wananchi wa nchi zetu mbili daima wako hatua mbele yetu. Wanafanya biashara zao kwa ubunifu mkubwa lakini sisi tunang'ang'ana na sheria na vikwazo na mambo kama hayo na tunawavuta

nyuma kidogo. Ni wakati sasa wa sisi viongozi kubadilika tuwe daraja la kuunganisha watu wetu na sio tuwe vikwazo kwao.

Mimi na ndugu yangu Rais Uhuru Kenyatta tumekubaliana kuweka utaratibu madhubuti wa kuzuia na kukabiliana na zile pilka pilka pale zinazotokea katika mipaka yetu wakati wa kuvusha biashara kwenda na kurudi katika nchi zetu mbili.

Waheshimiwa Spika, Maseneta na Wabunge mashirikiano ya uwekezaji na biashara ni sehemu tu ya mashirikiano mazuri kati ya nchi zetu. Utalii ni eneo nyingine ambayo tunapaswa kushirikiana sana. Kama nilivyogusia ekologia zetu zinaingiliana. Hivyo hivyo, ukaribu wa vivutio vyetu vya utalii na vyenyewe vinaingiliana.

Tunayo nafasi ya kunemeka pamoja ikiwa tutashirikiana katika sekta hii kuliko kushindana. Badala ya kunyang'anyana idadi ya watalii busara inatutaka tuelekeze nguvu zetu kuhamasisha mtalii aongeze idadi ya siku ambazo atazitumia nchini Kenya na Tanzania. Kwa kufanya hivyo, sote tutafaidika.

Kama alivyowahi kusema Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alisema na ninanukuu:

“Tukipoteza muda mwingi kugawana kibaba - kibaba ni kipimo cha kupimia kama mchele, ngano, sembe.”

Anasema tukipoteza muda mwingi kugawana hicho tutapoteza muda mzuri sana wa kuvuna kipimo kikubwa zaidi.

Mashirikiano yetu yanashamirishwa pia na jitihada kubwa tunazochukua katika vita dhidi ya uhalifu, ujangili, ugaidi, madawa ya kulevya na uharamia Bahari ya Hindi na katika Ziwa la Victoria.

Kwa vile muhalifu wa Kenya na Tanzania wana mashirikiano mazuri basi hakuna budi vyombo vyetu vya ulinzi na usalama navyo vishikamane na wawe na mashirikiano mazuri ili tuweze kulinda maeneo yetu na kushinda ushirikiano wa wahalifu.

Mashirikiano haya mazuri baina ya vyombo vyetu yamechangia sana kuwepo kwa utulivu na kutoa fursa kwa shule za kibiashara na uwekezaji kushamiri. Kenya ikiwa salama na sisi Tanzania tuko salama. Hali kadhalika, Tanzania ikiwa salama, Kenya nayo inakuwa salama.

Waheshimiwa Maspika, Maseneta na Wabunge, ujenzi wa miundo mbinu ya pamoja ni sehemu ya jitihada zetu za kuimarisha mashirikiano yetu ya kiuchumi na kimikakati. Miradi hii inajumuisha kwa uchache miradi ifuatayo: Kwanza ni ujenzi wa barabara ya lami kutoka Lamu-Mombasa kupitia Tanga-Bagamoyo hadi Dar es Salaam yenye urefu wa kilomita 454 chini ya programme ya Jumuiya ya Africa Mashariki ya kuendeleza miundo mbinu ya bara bara kwa nchi za Jumuiya ya Africa Mashariki. Katika ushorodha wa pwani - yaani coastal corridor - kwa upande wetu tuko mbioni kukamilisha ujenzi wa kipande cha Pangani-Bagamoyo na barabara za lami zenye urefu wa kilomita 124.5.

Tayari tumekwisha pata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Jana nilikuwa na mazungumzo na kaka yangu Uhuru naye anamalizia mazungumzo ya kupata fedha ili kazi hii ianze kwa upande wa Kenya na tukutane pale kwenye mpaka.

Mradi wa pili ni barabara ya Arusha-Holili-Taveta-Voi, yenye urefu wa kilomita 260. Mradi huu ni sehemu ya mradi wa maendeleo ya barabara ya Arusha-Namanga-Athi

River iliyofunguliwa rasmi mwaka wa 2002. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza imeshakamilika, sasa tunajipanga kuendelea na awamu ya pili ya mradi huu.

Mradi wa tatu, tunavyo vituo vya huduma vya pamoja mpakani vya Namanga: Namanga West BP na Holili Taveta West BP. Vituo hivi vimerahisisha shughuli za biashara mipakani na uvukaji wa watu.

Nafurahi kuona vituo hivi vimekuwa chachu ya shughuli za kiuchumi katika maeneo ya mipaka ya mipaka yetu. Tunaendela na mchakato wa kukamilisha mifumo ya vituo vya Horohoro, Lunga Lunga na Sirari-Isebania ili navyo viweze kutoa huduma kwa wepesi na kwa ufanisi.

Mradi wa nne ni wa kusafirisha umeme mkubwa wa Kw400. Kwa upande wa Tanzania mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme kutoka Singida hadi Namanga. Ujenzi wa kituo kipya cha kuposia umeme mjini Arusha na eneo la Legumori na upanuzi wa kituo cha kuposia umeme cha Singida.

Kwa upande wa Kenya, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa KW400 inayojengwa kutoka kituo cha kupozia umeme cha Isinya hadi Namanga yenye urefu wa kilomita 94, inayounganishwa na njia ya umeme inayojengwa upande wa Tanzania. Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na Shirika la Maendeleo la Japan, zimekubali kugharamia miradi hiyo.

Mradi mwigine – Mwenyezi Mungu akijalia *Inshallah* - Serikali zetu mbili zitaanza kutekeleza mradi wa bomba la gesi, kutoa gesi Dar es Salaam hadi Mombasa. Mazungumzo ya kutafuta fedha kwa ajili ya mradi huo yanaendelea. Tunatarajia yatakamilika mapema inavyowezekana.

Ndugu zangu Maseneta na Wabunge wa Bunge la Kitaifa, mtakubaliana na mimi kuwa, kwa ukubwa wa miradi hii, gharama na muundo wake unalazimisha nchi zetu mbili kushirikiana kujenga miradi hiyo. Ni ishara tosha kuwa uhusiano wetu si wa kuishia kesho, kesho kutwa wala mtondogoo. Serikali zetu zinafanya uwekezaji huo kwa kuamini kuwa uhusiano wetu uko vizuri na utaendelea kuwepo daima.

Hivi ndivyo majirani na ndugu walioshibana wanavyoishi. Yeyote anayefikiria ama kudhamiria kuleta uhasama baina yetu, ujumbe kwao ni kuwa, Tanzania na Kenya tulikuwepo, tupo na tutaendelea kuwepo. Iwe kiangazi; iwe masika, Tanzania na Kenya tupo.

(Heko)

Waheshimiwa Maspika, Maseneta na Wabunge wa Bunge la Kitaifa, sote tunafahamu kwamba, dunia inakabiliwa na janga kubwa la ugonjwa wa Korona ambalo limeathiri kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zetu. Limepelekea kwa sehemu kubwa kutulazimisha kubadili mfumo wetu wa maisha.

Asubuhi nilikuwa nikiongea na wafanyi biashara nikawaambia kuwa, hivi tunavyoishi sasa hivi wote tukiziba midomo na pua, huko nyuma kabla ya Korona kuja, na kule vijijini mwetu, mtindo huu tulikuwa tunawafanyia mbuzi ili wasile mazao ya watu njiani. Leo Korona imebadilisha mfumo wa maisha. Wanadamu ndio tunaofifunga. Huyu ni adui kwetu.

Tunatambua kwamba kila nchi - ikiwemo Tanzania - imejiwekea utaratibu wa kupambana na janga hili kulingana na mazingira yake mahsusi na hali ya kusambaa kwa ugonjwa huo katika nchi hizo.

Niliwaeleza Watanzania katika Hotuba yangu katika Bunge la Nchi yetu - na ninapenda kurejelea hapa – kwamba, sisi Tanzania sio kisiwa. Tunaishi kama sehemu ya familia ya jumuiya ya kimataifa. Kwa hivyo, kupitia Kamati ya Wataalamu niliyoiunda, tumeanza mchakato wa kutafakari mbinu zaidi za kukabiliana na janga hili.

(Heko)

Tunapoendelea kusubiri mapendekezo ya wataalamu na hatua za kuchukua tahadhari zote, ikiwemo kusitisha baadhi ya safari kwenye maeneo ya mikurupuko zinachukuliwa. Kwa vyovyote vile itakavyopendekezwa, nina hakika kuwa lazima tushirikiane na jirani zetu ikiwemo Kenya katika kukabiliana na janga hili.

Mapambano dhidi ya janga hili yanapaswa kutuleta pamoja na sio kutufarakanisha. Ni imani kwamba tukiweka jitihada na maarifa yetu pamoja, tutakabiliana na janga hili bila uoga. Tutashinda na maisha ya wananchi wetu yataendelea kuwa ya kawaida huku tukichukua athari za kutosha.

Waheshimiwa Maspika, Maseneta na Wabunge wa Bunge la Kitaifa, hatuwezi kuelezea uhusiano wetu vizuri bila kutambua uhusiano wa Mabunge yetu ya nchi mbili. Umekuwa ni uhusiano mzuri wa majira yote. Ninatumia fursa hii kufikisha kwenu shukrani za dhiti na salamu kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote kwa kuungana nasi na kutufaraji katika kipindi kugumu cha msiba wa hayati mpendwa wetu Rais (Dr.) John Pombe Magufuli. Mlitufuta machozi na kutufaraji sana.

Tuliguswa sana na uamuzi wa Bunge la Seneti kupitia Kikao chake cha Machi, 24, 2021 kujadili na kusajili kwenye kumbukumbu za Bunge salamu maalum za rambirambi kufuatia kifo cha hayati Rais (Dr.) Magufuli. Tunawashukuru sana.

Nafahamu pia viongozi wa mihimili mitatu ya Serikali ya Kenya, ukiwemo wewe Mheshimiwa Spika wa Bunge la Taifa, na Spika wa Seneti, Mheshimiwa Kenneth Lusaka, mlitembelea makazi ya balozi wetu kutoa salamu za pole. Sisi Watanzania tulifarajika sana kwa kuwa nasi wakati wa majonzi. Hatuna la kuwalipa ndugu zetu Wakenya, zaidi ya kusema Mungu awabariki sana.

Wakati wa msiba na dhiki ndio wakati unapomjua ndugu yako wa kweli na jirani zako wa majira yote. Mlitudhihirishia bila chembe na shaka kuwa, nyinyi ni ndugu zetu wa shida na raha. Asanteni sana.

(Heko)

Ndugu zangu, sisi ni wafuatiliaji wakubwa wa mikutano ya Bunge la Kenya. Mimi binafsi huwa ninapenda kusikiliza Bunge la Kenya. Tunafanya hivyo kwa kuwa yanayojadiliwa humu yanatuhusu. Bunge la Seneti na Bunge la Kitaifa la Kenya

zinatusisimua kwa mengi. Tunafurahia upana wa demokrasia yake, uzito wa mijadala na hamasa ya Wabunge wake.

(Heko)

Tulifurahishwa zaidi na uamuzi wenu wa kuanza kutumia lugha ya Kiswahili Bungeni. Ndicho kinachonifanya nisikilize Bunge la Kenya. *Ninaenjoy* Kiswahili kile. Kiswahili chenu kina vionjo vingi ambavyo peke yake ni burudani tosha kusikiliza.

(Kicheko)

Nilikuwa ninamsikiliza Mheshimiwa Spika anavyoshindwa kutaja namba za miaka kwa Kiswahili. Inafurahisha kwamba mmeshatunga Kanuni za Kudumu kwa Kiswahili na Mkamwalika Mheshimiwa Job Ndugai kuja kusizindua Oktoba, 31, 2019. Hili linatia moyo kwamba tuko pamoja na kweli mnataka kutumia Kiswahili, lakini hatua kwa hatua.

(Kicheko)

Ndungu zangu Wabunge, rai yangu kwenu ni kuomba mtusaidie kulea uhusiano wetu mzuri. Ninasema hivyo nikitambua kwamba nyinyi ndio wawakilishi na sauti ya wananchi wa Kenya. Nyinyi ndio wenye dhamana ya kutunga sheria na kushauri Serikali juu ya mwelekeo wa sera na kuongoza wananchi wenu waliowachagua.

Dhima yenu katika kukuza ushirikiano baina ya nchi zetu mbili ni kubwa sana. Mnao uwezo mkubwa wa kuamua kasi ya ushirikiano wetu iwe ya haraka ama ya kusuasua kwa aina ya sheria mtakazotunga na sera mtakazopitisha.

Dira na mwelekeo wa Serikali ya awamu ya sita ninayoiongoza ni kudumisha mazuri ya awamu zilizopita, kuyaendeleza mema yaliyoko na kuleta mazuri mengine mapya. Nimekuja kuwaahidi kuwa chini ya uongozi wangu, mimi na wenzangu katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutafanya kila linalowezezana kuimarisha uhusiano kati ya nchi zetu mbili. Kama kuna jambo linalolegalega au kama uhusiano wetu unasuasua, basi nimekuja hapa Kenya ili kukazia yale ambayo yamelegalega. Nimekuja kuyanyoosha yale ambayo yalikuwa yamejipindapinda.

Leo mtasoma Kiswahili.

(Kicheko)

Waheshimiwa Spika, Maseneta na Wabunge wa Bunge la Kitaifa, Tanzania na Kenya ni wanachama na waasisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi zetu mbili ndizo zenye eneo kubwa kijiografia na idadi kubwa ya watu na milango pekee ya bahari kwa nchi zingine za Afrika Mashariki. Ukweli huu umekuja na wajibu na dhima kubwa kwa nchi zetu mbili.

Uhusiano wa nchi zetu mbili ukishamiri, Afrika Mashariki nzima itashamiri. Biashara kati yetu ikistawi, Afrika Mashariki nzima inastawi. Hivyo basi, hatuna budi nchi zetu mbili kutambua wajibu wetu na dhima yetu hiyo kwa upande huu Mungu alikotuambia, Afrika Mashariki. Tunapaswa tutambuwe kuwa kila mara panapotokea

kutoelewana kati yetu, tunadhohofisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bila kukusudia, tunajikuta pia tunaathiri kasi ya utangamano wa Afrika Mashariki; hivyo hatuna budi kuendelea kuelewana.

Nikiri kwamba kuna nyakati ambapo ushirikiano wa Afrika Mashariki ulijaribiwa, ambapo baadhi ya matukio, kauli na vitendo vyetu, viliweka majaribuni mahusiano yetu na kuupima uimara wa dhamira zetu za kuendelea na safari yetu ya utangamano. Ninachofarijika ni kwamba katika nyakati zote hizo, kwa busara za viongozi waliotutangulia, na kwa imara wa mafundi wa uhusiano wetu, tulishinda na dhamira yetu iliimarika zaidi. Uchungu wowote uliojitokeza pale ambapo tulijaribiwa, ulikuwa ni uchungu wa uzazi na sio uchungu wa maradhi. Kwa maana kwamba, uchungu wa uzazi unaishia kupata mtoto na kuleta furaha kwenye familia. Lakini uchungu wa maradhi unaishia kwenye kifo. Kwa hivyo sisi tunapokerana, uwe uchungu wa uzazi. Tukae, tuzungumze na tupate mtoto, amani, na tuendeleo na uhusiano wetu.

(Heko)

Niwahakikishie kuwa mimi na wenzangu nchini Tanzania tutafanya kila linalowezekana ili uhusiano wetu uzidi kungaa' na kwa kufanya hivyo, tung'arisha ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tanzania itaendelea kuwa jirani, pia na rafiki muaminifu wa Kenya na mwanachana muadilifu na wakutumainiwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jitihada zangu na wenzangu katika serikali ninayoiongoza zitaelekezwa katika kuimarisha ushirikiano wetu ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Tutaelekeza jitihada zetu katika kutafuta majawabu palipo na changamoto, kufufua fursa palipo na vikwazo na kuleta matumaini palipo na mashaka. Tutafanya hivyo kwa kuamini kwa dhati kabisa kuwa wana Afrika Mashariki hatima yetu imefungamana nasi hatuna budi tufungamane.

Ombi langu kwenu waheshimiwa wabunge kama nilivyosema awali, mtusaidie kutimiza adhima hiyo. Sisi tulioko serikalini, mtusukume tutekeleze wajibu wetu huu wadhimu na pale tunapo zuba, msisite kutukosoa. Nanyi pia tunawaomba mtimize waajibu wenu. Mtusaidie kutunga sheria na kushawishi serikali zetu kuhusu sera zinazochochea na kuwezesha mtangamano. Tusiruhusu na tukemee misimamo, mitazamo na kauli za baadhi ya wanasiasa ndani ya mabunge yetu ya kuleta mgawanyiko na kudhohofisha Jumuiya ya Afrika Masharika.

(Heko)

Daima, tuwatangulie wafanyabiashara na wananchi wetu katika utangamano na kuwaongoza badala ya wao wananchi wetu kutuongoza sisi. Yanayotokea sasa hivi ni kwamba wafanya biashara wako mbele kuliko sisi. Inabidi sasa tutunge sera na sheria kuendana na mwenendo wa wafanya biashara. Lakini inavyotakiwa, ni tutunge sera na sheria ili wafanya biashara wafuate sera na sheria zetu. Nasema hayo kwa sababu falsafa zinasema kuongoza ni kuonyesha njia na sio kufunga njia. Sisi kama viongozi wa serikali, mabunge na mahakama zetu tunapaswa kuonyesha wananchi wetu nji na tusiwafungie njia za maendeleo au ustawi wao.

(Heko)

Waheshimiwa Maspika, Maseneta na Wabunge wa Bunge la Taifa, nitimisha hotuba yangu kwa kusema kwamba kama mnavyojua, moyo ukilemewa na furaha, furaha ya moyoni hutoka mdomoni. Ningetamani kuendelea kuzungumza nanyi kwa kirefu zaidi, kueleza furaha yangu kwa upendo mkubwa mlionionyesha, ukarimu mkubwa mliotufanyia mimi na ujumbe wangu na heshima kubwa mlionipa. Isitoshe, tunapokutana Tanzania na Kenya, tunakuwa na maneno mengi sana ya kuzungumza, hayaishi. Hii ni kutokana na ukubwa na uzito wa uhusiano wa nchi zetu mbili. Sitaki kusema naishia hapa bali mniruhusu ni ahirishe maneno yangu hapa.

(Heko)

Nitakuja kusema maneno mengine mbele tukikutana. Kwa hivyo siishi hapa bali nahairisha maneno yangu hapa. Tunapokutana Watanzania na Wakenya, kuna mambo mengi; utani unakuwa humo na vijembe viko humo. Hayo ndiyo mambo yanayochangamsha uhusiano wetu. Sina shaka kuwa tutapata fursa ya kuyazungumza mengi zaidi na kwa kina katika majukua mengine tutakayokutana.

Natumia fursa hii kwa mara nyingine tena kuwashukuru waheshimiwa maspika kwa mara nyingine tena kwa kunikaribisha. Lakini namshukuru Rais Uhuru Kenyatta kwa mwaliko wa kuniomba mimi kufanya ziara hii rasmi ya kiserekali nchini Kenya. Nataka niwadhibitishie kwamba tumevuna mengi na makubwa sana katika ziara hii. Ziara hii imefungua milango mingi sana. Lililobaki, mtusimamie kwenye utekelezaji.

Nami nimemualika Rais Uhuru Kenyatta aje Tanzania mwezi wa Desemba mwaka huu. Tanzania itatimiza miaka 60 ya uhuru mwaka huu. Nimemualika Rais Uhuru Kenyatta aje kwenye sherehe hizo kama mgeni wetu maalum.

Kama nilivyosema, natumia fursa hii kuwashukuru maspika; Mhe. Kenneth Lusaka na Mhe. Justin Muturi kwa makaribisho yenu mazuri sana ndani ya bunge. Nawashukuru pia Maseneta na wabunge wa Bunge la Taifa kwa kutenga muda wenu adhimu kunikaribisha kuzungumza nanyi. Kupitia kwenu, nawashukuru ndugu zetu, wananchi wa Kenya kwa mapokezi mazuri waliotupatia. Tunaondoka Kenya na kumbukumbu nzuri ya ziara hii na shauku kubwa ya kurudi tena siku zijazo.

Hii ni ziara yangu ya kwanza nchini Kenya, nawaahidi kuwa haitakuwa ya mwisho. Kwa maana hiyo, nasema, udumu undugu wa Kenya na Tanzania na wadumu viongozi wetu. Mungu aibariki Jamhuri ya Kenya. Mungu aibariki. Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

(Heko)

ADJOURNMENT

Spika wa Seneti (Mhe. Lusaka): Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Spika wa Bunge la Taifa, Maseneta na Wabunge wa Bunge la Taifa, ni wakati sasa wa kuhairisha kikao cha Seneti hadi kesho, Alhamisi, tahere sita, Mei, mwaka wa 2021, saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Seneti.

Asanteni sana.

(Heko)

The Speaker of the National Assembly (Hon. Muturi): Your Excellency Hon. Samia Suluhu Hassan, the President of the United Republic of Tanzania, Speaker of the Senate, Hon. Kenneth Lusaka, Members of the National Assembly and Senators. It is now my pleasure to announce the adjournment of this House until Thursday, 6th May, 2021 at 10.00 a.m.

(Applause)

**DEPARTURE OF HER EXCELLENCY THE PRESIDENT OF
THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

*(Hon. Members and Senators rose in their places while
Her Excellency the President of the United Republic of Tanzania
(Hon. Samia Suluhu Hassan) left the Chamber)*

Parliament rose at 3.50 p.m.